# DARUBINI

# Uelekeo wa Uwajibikaji katika Upatikanaji Rasilimali Tanzania: Kuimarisha Ushiriki katika Majukwaa ya Kimataifa




©IPIS

Toleo la 6
Oktoba 2024

Imedhaminiwa na: Belgium partner in development

Imechapishwa na:
HakiRasilimali, International Peace Information Services (IPIS),
Business Human Rights Tanzania (BHRT) & Avocats Sans Frontières (ASF)

# Uelekeo wa Uwajibikaji katika Upatikanaji Rasilimali Tanzania: Kuimarisha Ushiriki katika Majukwaa ya Kimataifa

## Utangulizi

Uelekeo wa kimataifa juu ya uwajibikaji wa kibiashara, hasa katika sekta ya uziduaji, umeongeza mijadala mikubwa katika maswala ya haki za binadamu na miongozo ya kiuwajibikaji katika mnyororo wa ugavi wa madini. Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD) limechukua jukumu kubwa katika kuchagiza mijadala, na kuandaa miongozo ya utathmini wa kina kwa lengo la kuimarisha mwenendo wa uwajibikaji wa kibiashara na uwajibikaji katika mnyororo wa ugavi wa madini. Miongozo hii inalenga moja kwa moja katika kusaidia makampuni kuzuia vitendo vinavyochangia na kupelekea migogoro, ukiukaji wa haki za binadamu, vilevile hata vitendo vya uhalifu wa kifedha.

Toleo hili la DARUBINI linasisitiza umuhimu wa majukwaa ya kimataifa yenye mjumuiko wa wadau mbalimbali hasa katika majadiliano yanayohusu miongozo ya kiuwajibikaji katika upatikanaji wa rasilimali ambayo ni suluhu katika changamoto za haki za binadamu, athari za kimazingira, n.k. Toleo hili limeangazia kwa kina hasa ushiriki wa serikali katika kupelekea na kuchochea miongozo, kanuni na viwango vya uwajibikaji katika mnyororo wa ugavi wa madini. Vilevile toleo hili limejumuisha sauti za jamii zinazo ibua na kutoa picha halisi kuhusu masuala ya haki za binadamu katika shughuli zinazo fanyika ndani ya sekta ya uziduaji.

## Nafasi ya Tanzania katika Sekta ya Madini duniani

Tanzania ni nchi iliyojaliwa rasilimali nyingi, miongoni mwa hizo ni futi za ujazo trilioni 57 za gesi asilia, wakia milioni 45 za dhahabu, na uwepo wa hifadhi nyingi za madini ya almasi, tanzanite, shaba na nikeli. Tanzania inashika nafasi ya nne kwa uzalishaji wa dhahabu barani Afrika baada ya Afrika Kusini, Ghana, na Mali, huku takwimu zikionesha inazalisha asilimia 1.3 ya uzalishaji wa dhahabu duniani . Pamoja na uchimbaji madini kuwa sehemu muhimu ya uchumi wa Tanzania, Uwekezaji wa ndani na uwekezaji unaotoka nje ya nchi yote kwa pamoja umekua ni sehemu ya vyanzo muhimu vya mapato ya mauzo ya nje na maendeleo ya kiuchumi. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha wa 2021/22 , mauzo ya dhahabu yalizalisha dola bilioni 2, ikifuatiwa na shaba $ 183 milioni, na almasi $ 56 milioni. Aidha, shughuli hizi za uchimbaji madini kwa namna yake hufungamana na hatari na changamoto mbalimbali, ikiwemo hatari na changamoto ya ukiukwaji wa haki za binadamu, uharibifu wa mazingira, na changamoto za kifedha – Na haya yote yame ainishwa na kuangaziwa katika muongozo wa tathmini ya kina ulio tolewa na OECD.

Ushiriki wa kikamilifu kwa Tanzania katika majukwaa ya kimataifa ikiwemo Jukwaa la OECD linalo angazia hasa katika maswala ya Mnyororo wa Ugavi wa Madini, ni muhimu kwa ajili ya kupunguza hatari na changamoto hizi za ukiukaji wa haki za binadamu, uharibifu wa mazingira, na changamoto za kifedha kwa lengo la kukuza uwajibikaji katika sekta ya madini.

## Mijadala Inayohushisha Wadau Mbalimbali Kuhusu Uwajibikaji Katika Mnyororo wa Ugavi wa Madini.

Katika kushughulikia changamoto zilizopo katika mnyororo wa ugavi wa madini inahitaji ushirikiano wa kimataifa na mazungumzo yanayo jumuisha wadau mbalimbali. Vilevile, majukwaa ya kitaifa na kikanda yana waleta wadau muhimu ikiwemo serikali, mashirika ya kimataifa, Asasi za kiraia, sekta binafsi na wadau wengine ili kujadili kwa kina katika kukabiliana na changamoto zilizopo. Mipango na miongozo ya kimataifa kama vile OECD, pamoja na mifumo mbalimbali ikiwemo mifumo ya uwazi katika sekta ya uziduaji (TEITI), Kwa ujumla wake mambo yote haya yanatoa mchango muhimu katika kukuza uwazi na uwajibikaji katika kiwango cha kimataifa.

Kwa kuzingatia viwango vya kimataifa, nchi za Kiafrika zinazozalisha madini kama vile Tanzania zinaweza kuhakikisha kuwa utajiri wa rasilimali uliopo unakua ni chachu ya kuleta maendeleo endelevu huku mahitaji ya jamii husika yakishughulikkiwa. Majukwaa haya yanayo wajumuisha wadau wengi ni muhimu sana katika kubainisha mapungufu ya kisera yaliyopo, na mifano hai ya kiutekelezaji kwa kujifunza kutoka katika nchi mbalimbali, ili kuongeza hali ya uwajibikaji, usawa na usimamizi mzuri wa rasilimali.

## Uwakilishi wa Tanzania katika Jukwaa la OECD Linalo Angazia Uwajibikaji katika Mnyororo wa Ugavi wa Madini.

Licha ya nafasi yake kubwa katika soko la madini duniani, ushiriki wa Tanzania katika Jukwaa la OECD unaonekana kubadilika badilika. Mwaka 2009 , Tanzania ilihusika katika kuandaa Miongozo ya Tathmini ya Kina katika Mnyororo wa Ugavi wa Madini hasa katika Maeneo Hatarishi na yenye athari za kimigogoro. Aidha, katika kipindi cha karibuni hasa katika jukwaa la OECD mfano mwaka 2023 na 2024, uwakilishi wa serikali ya Tanzania umekuwa ni mdogo.

Katika kongamano la hivi karibuni la 2024, uwakilishi wa Tanzania ulionekana kujumuisha Benki Kuu ya Tanzania (BoT), kampuni za kusafisha madini kama vile Kiwanda cha Kusafisha dhahabu cha Geita, na baadhi ya Asasi Za Kiraia (CSOs) kama vile HakiRasilimali. Hata hivyo, maofisa wa Wizara ya Madini hawakauonekana katika mijadala iliyokuwa ikiendelea katika jukwaa hilo ambalo HakiRasilimali walihudhuria.

Ushiriki huu mdogo unaibua wasiwasi na unafikirisha kwa maana kama taifa linaweza kukosa mijadala muhimu kuhusu madini mkakati, uwajibikaji wa kibiashara, na namna ya udhibiti wa mambo hatarishi yanayo husiana na shughuli za uchimbaji madini.

Mjadala mkuu katika Jukwaa la OECD la 2024 ulilenga hasa kujadili changamoto zilizopo katika mnyororo wa ugavi wa madini mkakati na umuhimu wake katika mpito wa nishati. Mada nyingine muhimu ni pamoja na ushiriki wa jamii za kiasili katika maamuzi ya kiuwekezaji, kutokuwepo kwa shuruti na ulazimishaji, kuwepo kwa uwelewa wa awali na hali ya kufahamishwa, pamoja na uhitaji wa uwepo wa mifumo madhubuti ya uwasilishaji malalamiko tena iliyohuru na yenye haki. Hivo basi, yafuatayo ni maswala muhimu ambayo kama Tanzania yana husiana nayo kutoka katika jukwaa hilo la OECD la 2024.

## 1. Haki za Binadamu na Mifumo ya Uwasilishaji Malalamiko

Huu ni mjadala muhimu sana uliolenga katika kuimarisha mifumo ya uwasilishaji malalamiko ili kulinda jamii zilizoathiriwa na shughuli za uchimbaji madini. Kama Tanzania hili ni swala linalo jitokeza na kuripotiwa mara kwa mara, hasa katika maswala ya ukiukwaji wa haki za binadamu kutokana na shughuli za uchimbaji madini. Katika miaka ya hivi karibuni, kampuni kama vile EACOP, Barrick na Petra Diamonds zimekuwa zikianzisha mifumo ya kuwasilisha malalamiko, na kwa namna yake ni muhimu kutathmini, kufuatilia, na kuendelea kujadili utendaji kazi wa mifumo hii na kuhakikisha kwamba inaendana na kanuni za kimataifa. Hali ya utathmini na ufuatiliaji itasaidia kuimarisha ufanisi wa mifumo hiyo katika kushughulikia matatizo ya jamii, kuboresha uwajibikaji, na kuendeleza shughuli za uchimbaji madini kufanyika kwa hali ya uwajibikaji.

## 2. Uchimbaji na Mtiririko Haramu wa Dhahabu barani Afrika:

Wataalamu katika Kongamano hilo walisisitiza hitaji kubwa la kuwa na kanuni kali na njia bora zaidi za utekelezaji ili kushughulikia swala la uchimbaji haramu, hasa madini ya dhahabu. Kwa Tanzania, nchi inayoongoza kwa uzalishaji wa dhahabu barani Afrika, mijadala kama hii ni muhimu katika kuhakikisha dhahabu inapita katika njia halali, yenye uwazi na kuhakikisha kuwa jamii zinazo patikana katika maeneo ya uchimbaji zinanufaika na shughuli za uchimbaji madini. Licha ya yote hayo, bado ushirikiano wa kimataifa ulisisitizwa kutokana na umuhimu wake katika kuzuia biashara haramu ya madini inayofanyika kwa kujumuisha mipaka ya nchi mbalimbali.

## 3. Unyeti wa Swala la Hali ya Hewa katika Shughuli za Uchimbaji Madini:

Wakati dunia inaelekea katika matumizi ya nishati safi, jukwaa lilitumia nafasi hio kusisitiza vitendo vya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa katika sekta ya uziduaji. Mijadala kuhusu madini mkakati imeonesha fursa kubwa sana kwa Tanzania, kwasababu madini hayo ni muhimu sana katika uwepo wa teknolojia ya nishati mbadala. Kwa kutegemea hifadhi kubwa ya madini muhimu na madini mkakati kama vile kobalti, nikeli, graphite, na madini ardhi adimu, Mijadala hii inaonesha kuwa kuna nafasi kubwa ya Tanzania kunufaika kutokana na ushriki wao katika mijadala hio, hasa katika uhusiano wa shughuli za uchimbaji madini na swala la mpito wa nishati ulimwenguni.



## 4. Ushirikishwaji wa Jamii za Kiasili

Jukwaa hilo lilisisitiza umuhimu wa kushirikisha watu wanaotoka katka jamii za kiasili na kuzingatia kanuni za FPIC ili kuhakikisha jamii zinapewa taarifa kikamilifu na kushauriana kabla ya kuanza kwa shughuli za uchimbaji madini. Hili ni muhimu hasa kwa Tanzania, ambapo mashauriano duni yamesababisha migogoro, watu kuhama na kugawana faida bila haki. Kuimarisha ushirikishwaji wa jamii na kutekeleza kanuni za FPIC ni muhimu kwa ajili ya kuendeleza usawa na maendeleo endelevu ya uchimbaji madini ambayo yanathamini na kuheshimu haki za jamii zinazo patikana katika maeneo ya uchimbaji.

## 5. Ushirikiano wa Kimataifa na Uwajibikaji wa Uchimbaji:

Jukwaa hilo lilisisitiza kuwa ushirikiano wa kimataifa ni muhimu kwa maendeleo endelevu katika sekta ya madini. Muundo Mzuri wa ushirikiano kati ya serikali, viwanda, na asasi za kiraia unatoa muongozo uliolenga kuboresha hali ya uwajibikaji katika ulimwengu. Aidha, jukwaa hilo limetilia mkazo juu ya kuwepo kwa makubaliano kimataifa ya kupambana na uchimbaji haramu wa madini, kuboresha usimamizi, kuimarisha uwazi, kuhakikisha hali ya uwajibikaji katika mnyororo wa ugavi wa madini kwa kuhakikisha kudhibiti hali ya ukiukaji wa haki za binadamu na athari za kimazingira.

## Je Kuna Ukosefu wa Fursa kwa Tanzania?

Kwa hivi karibuni, kulingana na ushiriki mdogo uliopo kwa Tanzania katika jukwaa la OECD, kuna hali ya ukosefu wa fursa kulingana na mijadala muhimu ya kimataifa kuhusu uwajibikaji katika mnyororo wa ugavi wa madini. Kuongezeka kwa mahitaji na matumizi makubwa ya madini mkakati katika ulimwengu kunatoa fursa kubwa kwa Tanzania katika kushawishi na kuchangia upatikanaji wa sera zinazoweza kuinufaisha sekta hii inayo ibukia. Ushiriki huu mdogo, unapelekea kwa nchi kukosa fursa ya kutetea maslahi yake, kushughulikia masuala ya haki za binadamu, na kuweza kujifunza mifano mizuri kutoka kwa nchi zilizo endelea kwa lengo la kufikia maendeleo endelevu.

Kukosekana kwa wawakilishi wakuu wa serikali, hasa kutoka Wizara ya Madini, kunatoa taswira ya changamoto za kiusimamizi hasa katika uandaaji wa mikakati madhubuti kwa maendeleo ya sekta ya madini. Mijadala muhimu iliyo fanyika katika kongamano hilo ni kama vile hatari za kimigogoro, uwajibikaji wa uchimbaji, na mabadiliko kuelekea uchumi wa kijani. Haya yote ni maeneo ambayo Tanzania ingeweza kuchangia ipasavyo, ikajiweka kama kiongozi katika uwajibikaji wa uchimbaji madini huku ikijihakikishia manufaa ya muda mrefu kwa uchumi wake na jamii kwa ujumla.



Katika dunia ya leo yenye muingiliano, ushiriki madhubuti wa Tanzania katika majukwaa ya kimataifa kama vile OECD ni muhimu katika kuunda na kushawishi uwepo wa miongozo ya uwajibikaji wa mnyororo wa ugavi wa madini na kuhakikisha kwamba utajiri wa rasilimali zilizopo zinachangia na kupelekea maendeleo endelevu. Kwa uwakilishi na ushiriki madhubuti, Tanzania inaweza kulinda vema maslahi yake, kukuza uwajibikaji katika shughuli za kibiashara, na kuongeza manufaa ya rasilimali zake kwa raia.

## Sauti za Jamii: Wasiwasi Unaoongezeka Kuhusu Ukiukwaji wa Haki za Binadamu katika Mnyororo wa Ugavi wa Madini Tanzania

Ukuaji wa uchumi Tanzania pamoja na uchimbaji wa rasilimali umeibua hatari kubwa hasa katika muktadha wa haki za binadamu na mazingira. Ripoti ya Haki za Binadamu na Biashara kwa Mwaka 2023/24 iliyo tolewa na kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) imeangazia jinsi shughuli na vitendo vya makampuni zinavyoathiri jamii, huku shughuli za uchimbaji madini na viwanda zikichangia kwa kiasi kikubwa ukiukwaji huu.

Ripoti hiyo imebainisha kuwa asilimia 46% ya Watanzania waliohojiwa wanaona ukiukwaji wa haki za kazi kwa kiasi kikubwa hutokea sana kwa upande wa makampuni, ikifuatiwa na uchafuzi wa mazingira ambayo ni asilimia 39%. Zaidi ya hayo, asilimia 17% ya Watanzania waliohojiwa walionesha wasiwasi wao kuhusu kukosekana kwa haki na upatikanaji nafuu, hasa katika kesi zinazohusu makosa ya makampuni. Mathalani, kesi ya Kampuni ya chokaa ya Maweni mkoani Tanga, ambapo wakazi wameripoti athari kubwa za kimazingira kutokana na uendeshaji wa kampuni hiyo. Mkazi wa eneo hilo alilaumu hali hiyo, akisema:

> **"Uendeshaji wa Kampuni ya Maweni Limestone una athari kubwa ya kimazingira katika maeneo yetu ya makazi. Niliweka bati mpya hivi karibuni, na tayari zimefunikwa na vumbi. Kama Uchafuzi huu wa vumbi unatokea kwa wingi hivi sasa, Je, itakuwaje kwa jamii katika kipindi cha miaka sita?"**

Uwepo wa vumbi jingi la viwandani ni mfano mmoja tu wa uharibifu mkubwa wa mazingira unaoathiri hali ya afya kwa jamii.

Huko Mtwara, uchimbaji wa makaa ya mawe umeibua wasiwasi mkubwa kuhusu uchafuzi wa hewa katika mazingira, huku vumbi la makaa ya mawe likiwa na hatari kubwa kiafya. Meneja wa Kanda ya Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) alizungumzia swala hilo, akitolea mfano malalamiko ya wafanyakazi wa TANESCO. Alisema,

> **, 'Watumishi wa TANESCO wametuletea tatizo la uchafuzi wa mazingira kutokana na vumbi la makaa ya mawe. Waliripoti kiwango kikubwa cha vumbi kutoka katika shughuli za viwandani, jambo ambalo linaweka afya zao pamoja na afya za watu wengine hatarini. Wametuhimiza kuchukua hatua za haraka".**

Changamoto hizi zinazo sababishwa na makampuni zinaonesha umuhimu mkubwa na uhitaji wa tathmini ya kina katika sekta ya rasilimali madini, mafuta na gesi Tanzania. Yote haya ni kwa lengo la kuendana na viwango na miongozo ya kimataifa kama ile iliyowekwa na OECD. Licha ya kuwepo na kupitishwa kwa miongozo ya kimataifa, baadhi ya makampuni nchini yanaendelea kudorora katika kuendana na viwango hivyo vya hiari na kusababisha uchafuzi mkubwa wa mazingira na ukiukaji wa haki za binadmu.

HakiRasilimali mara kwa mara huwa na vikao na majadiliano ya mambo mbalilmbali katika sekta ili kushauri na kutoa mapendekezo kwa lengo la kushughulikia maswala muhimu yanayo ikumba sekta ya madini, mafuta na gesi. Wakati wa kikao cha robo ya tatu, mambo mbalimbali yalijadiliwa ikiwemo mapungufu ya kisheria, maswala yanayoendelea kuhusiana na fidia, upatikanaji wa nafuu, na mchakato wa uandaaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Biashara na Haki za Binadamu. Kamishna kutoka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) alibainisha kuwa, Mpango huu "NAP" "utatumika kama chombo na muongozo wa kitaifa katika kutekeleza Kanuni za Umoja wa Mataifa za Biashara na Haki za Binadamu". NAP inakusudia kufafanua kwa uwazi majukumu na wajibu wa serikali, makampuni, na asasi za kiraia katika kulinda haki za binadamu katika shughuli za kibiashara.


©HakiRasilimali

Wakati Tanzania inaendelea kujikita katika lengo la kunufaika na utajiri wake mkubwa wa madini, kuna haja kubwa ya serikali kuongeza juhudi hasa katika ushirikiano wa sekta mbalimbali ili kukabiliana na hatari hizi za haki za binadamu na mazingira. Vilevile swala la uandaaji na utekelezaji wa mpango wa taifa kuhusu biashara na haki za binadamu itakuwa ni moja kati ya hatua muhimu katika kuhakikisha kuwa shughuli za makampuni zinaendeshwa kwa hali ya uwajibikaji na kuheshimu haki za binadamu. Kadhalika, ushiriki wa Tanzania katika majukwaa ya kimataifa kama vile OECD ni muhimu kwa ajili ya kuchangia hali ya uwajibikaji katika mnyororo wa ugavi wa madini kwa mustakabli wa maendeleo endelevu.

## Habari kwa Ufupi

1. Idadi kubwa ya wafanyakazi wa sekta rasmi hawana mikataba (The Citizen)
2. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imeandaa Kikao Kazi cha Mapitio ya Maandiko katika kipindi cha Uandaaji NAP (THBUB)
3. Tume yaanza ukusanyaji wa maoni kuhusu biashara na haki za binadamu (THBUB)
4. Serikali kuwafidia wanaohama kwa sababu ya kupisha miradi ya maendeleo (Habari Plus24 Media)
5. Wananchi wanaohama kwa sababu ya kupisha miradi, kupata fidia ni haki yao (MNEWSTZ BLOG)
6. Wananchi wanaohama kwa sababu ya kupisha miradi, kupata fidia ni haki yao (HABARI MSETO)
7. Tanzania inapanga marekebisho ya sheria ya madini ili kudhibiti magendo na vifo (The Citizen)
8. UN yasisitiza haki za binadamu kabla ya mkutano Septemba (The Guardian)
9. Upanuzi wa North Mara: Uchunguzi wa haki za binadamu unatupilia mbali madai ya kufukuzwa kwa NGO ya Kanada (IPP)